# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


**Tarehe: Februari 13, 2018**

## TAMKO DHIDI YA UKIUKWAJI WA UTAWALA WA SHERIA

Katika kuhakikisha kuwa haki za binadamu na utawala wa sheria vinaheshimiwa na kulindwa nchini Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeendelea kufanya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa serikali.

Kupitia utendaji kazi wa Serikali tumeona juhudi mbalimbali za kuboresha ustawi wa maisha ya wananchi ikiwemo kuwakutanisha wananchi na kusikiliza na kuweka mikakati bora ya kutatua kero zao. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua mchango wa mikutano baina ya viongozi na wananchi katika kutatua kero za wananchi na kinapongeza jitihada za viongozi mbalimbali wanaotekeleza wajibu huo.

Hata hivyo ombwe la viongozi wa serikali kutokufuata taratibu na sheria katika utekelezaji wa majukumu yao limeendelea kuathiri uhalali wa juhudi hizo. Kupitia mkutano wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndugu Paul Makonda na wananchi wa Dar es Salaam uliofanyika Februari 10, 2018, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimebaini mapungufu kadhaa ambayo yamekuwa yakifanywa si tu na Ndugu Makonda pekee bali pia na baadhi ya viongozi wengine wa serikali. Baadhi ya mapungufu ya kisheria yaliyotokana na mkutano huo ni pamoja na:

1. **Kusimamisha Utendaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata Kinyume na Sheria;** kwa mujibu wa Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi (2002). Mabaraza ya Ardhi ya Kata yameundwa kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi ya kata. Mabaraza hayo hupatikana kutokana na Kamati ya kata kupitia kikao cha maendeleo ya kata kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mabaraza ya Kata, 1985 Kifungu cha 4(1a). Kifungu cha 167 (1d) cha Sheria namba 4 ya Ardhi, 1999 kinayatambua mabaraza ya kata kama mahakama za ardhi kwa ngazi ya kata. Sambamba na sheria hizo, Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro namba 216, 2002 kinayatambua mbaraza ya kata kama mahakama ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa ngazi ya kata.
   Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi inamtaja Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa na mamlaka juu ya Mabaraza ya Ardhi ya Kata. Kwa mujibu wa sheria hizi Wakuu wa Mikoa hawana mamlaka ya kusimamisha, kuendesha wala kulekeza utendaji wa mabaraza ya kata katika mikoa yao. Hivyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kuwajulisha wananchi kuwa kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni batilifu na isiyokuwa na mashiko kisheria.


**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson,
Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member,
Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member

2. **Kuingilia muhimili wa Mahakama:** Ibara ya 107A – (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema "Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni Mahakama". Ibara ya 107 B inasisitiza uhuru wa mahakama katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa mujibu wa Ibara hii mihimili mingine ya dola na watendaji wake hawapaswi kwa namna yoyote ile kuingilia utendaji wa mahakama. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshuhudia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndugu Paul Makonda akishambulia utendaji wa Mahakama kinyume cha Katiba aliyoapa kuilinda. Ndugu Makonda amesikika mara kwa mara akitoa kauli za kushambulia na kukebehi utendaji wa mahakama na amerudia katika mkutano wake wa Februari 10, 2018 akisema "Mahakama haitaki kuguswa kwa kisingizio cha muhimili mwingine, wamechukua nafasi ya Mungu na mimi ni mteule wa Mungu lazima niwaseme".

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinawakumbusha viongozi wa serikali na wanasiasa kuwa hawana mamlaka ya kisheria kuingilia utendaji kazi wa mahakama wala kuelekeza utendaji wa Mahakama badala yake wanapaswa kuheshimu na kufuata taratibu za kimahakama katika upatikanaji wa haki.

**Mapendekezo:**

Kwa kutambua uwepo wa changamoto za kiuwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma na changamoto za kiutendaji katika mfumo wa utoaji haki nchini, Kituo cha Sheria na Haki za tunatoa mapendekezo yafuatayo ili kulinda utawala wa sheria nchini:

1. Serikali kufuata taratibu za kisheria katika kutatua kero na changamoto mbalimbali; watendaji wa serikali hasa katika nafasi za kisiasa wanapaswa kuacha kutumia mbinu za kisiasa, badala yake wanapaswa kufuata taratibu zilizopo kisheria ili kutatua changamoto na kero za wananchi kwa maendeleo endelevu.

2. Viongozi wa kisiasa kuacha kutumia mamlaka yao majukwaani kuwajibisha watumishi wa umma na badala yake kufuata taratibu kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002.

3. Watendaji wa serikali kuheshimu muhimili wa Mahakama; viongozi wa serikali wameapa kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muaungano wa Tanzania ambayo kupitia ibara ya 107 inaipa mahakama mamlaka ya juu kabisa katika utoaji haki. Viongozi wa Serikali hawapaswi kufanya kazi za mahakama kwani kwa kufanya hivyo wanaondoa imani ya wananchi kwa muhimili wa mahakama na kupelekea ucheleweshwaji wa haki.

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson,
Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member,
Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member

4. Serikali inapaswa kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata ili kuboresha ufanisi wa mabaraza hayo katika kuwafikia wananchi.

5. Serikali kufanyia kazi mapendekezo ya tafiti mbalimbali ili kuboresha utendaji wa vyombo vya utoaji haki kwa lengo la kurahisisha upatinaji wa haki. Mfano Utafiti uliofanywa na LHRC, 2004 juu ya Ufanisi wa Mabaraza ya Kata kwa Dar es Salaam na Pwani.

6. Mahakama inapaswa kutanua wigo katika utoaji elimu kwa umma ili kuwezesha wananchi kufahamu na kufuata njia sahihi za utoaji haki.

7. Wananchi kujifunza na kufuata mifumo sahihi ya utoaji haki; wananchi wanapaswa kutambua kwamba mahakama ndio muhimili wenye mamlaka ya juu ya utoaji haki kwa mujibu wa Katiba.

Mwisho, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua madhaifu yaliyopo katika vyombo vya usimamizi wa sheria na utoaji haki na kinaitaka serikali kutatua changamoto hizo ili kurahisisha upatikanaji wa haki badala ya kutumia changamoto hizo kama mtaji wa kisiasa.

**Imetolewa na;**

**Bi. Felista Mauya**
**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson,
Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member,
Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member